

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA TANO

23 MEI, 2018



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA TANO – TAREHE 23 MEI, 2018

I. DUA:

II. TAARIFA YA SPIKA:

III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA NISHATI:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Taarifa ya Mwaka ya Hesabu za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) kwa mwaka wa Fedha 2016/2017.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

### **IV. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**297. MHESHIMIWA DAVID ERNEST SILINDE  
(MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza ajira kwa Watanzania waliohitimu Vytho bila kujali kada walizosomea ambao mpaka sasa wapo mitaani.

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**298. MHESHIMIWA NASSOR SULEIMAN OMAR  
(ZIWANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Uhakiki wa Vyeti

umeathiri Wafanyakazi wengi na wengine wamepoteza ajira zao:-

Je, ni Wafanyakazi wangapi wamepoteza ajira zao katika Sekta ya Elimu pekee.

### **WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

#### **299. MHESHIMIWA AZZA HILLAL HAMAD (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

• Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupeleka maji katika Sekondari ya Masegwa.

#### **300. MHESHIMIWA IGNAS ALOYCE MALOCHA (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kutokana na tatizo kubwa la ukosefu wa maji katika Mji Mdogo wa Muze, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ilipitisha mpango wake wa kuondokana na tatizo hilo kwa kuanzisha mradi mkubwa wa kuchukua maji toka Mto Kalumbaleza na kusambaza katika Vijiji vya Muze, Mlia, Mnazi mmoja Asilia, Ilanga, Mbwi Kalakala, Isangwa na Uzia:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili kutekeleza mradi huo.

### **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

#### **301. MHESHIMIWA LAMECK OKAMBO AIRO (RORYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Wilaya ya Rarya iliyoanzishwa mwaka 2007 ina ukubwa wa kilometa za mraba 9345 na idadi ya Watu wapatao 400,000 lakini inakabiliwa na tatizo la uhaba wa Watumishi katika Mahakama ya Mwanzo ya Kineri, Ryagoro, Obilinju na Shirati; hadi sasa Wilaya ya Rarya inatumia Mahakama ya Wilaya Tarime hali inayosababisha kesi kucheleva kusikilizwa kwa wakati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama ya Wilaya kwenye Jimbo la Rarya.

#### **302. MHESHIMIWA STEPHEN HILARY NGONYANI (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Katika Kata ya Magoma, Korogwe Vijijini kumejengwa Mahakama ya Mwanzo ya

Kisasa, lakini toka ijengwe imefikia miaka saba sasa haijafunguliwa:-

Je, ni lini Serikali itaifungua Mahakama hiyo ili Wananchi waachane na usumbufu wa kufuata huduma za Mahakama Korogwe.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**303. MHESHIMIWA JOHN JOHN MNYIKA (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara za Pete (*Ring roads*) na barabara za Mchepuko (*feeder roads*) ni muhimu katika kupunguza msongamano na matatizo ya miundombinu kwa Wananchi:-

- (a) Je, Serikali itakamilisha lini ujenzi wa barabara hizo zilizoanza kujengwa katika Jimbo la Kibamba;
- (b) Je, Serikali itaanza lini ujenzi wa barabara ambazo zimetajwa katika mipango ya Serikali lakini hazijaanza kujengwa mpaka sasa.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **304. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Imebainika kuwa baadhi ya Madereva wa bodaboda wamekuwa wakifanya ukatili kwa kufanya ubakaji, ulawiti na kuwapa baadhi ya Wanafunzi mimba:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti hali hii hasa kwa wale bodaboda wanao wahadaa baadhi ya Wanafunzi wa kike;
- (b) Je, ni Wanafunzi wangapi waliripotiwa kupewa mimba na bodaboda katika kipindi cha miaka 3 iliyopita.

## **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

### **305. MHESHIMIWA DESDERIUS JOHN MIPATA (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi Na Jeshi la Kujenga Taifa:- Wananchi wa Kata ya Nkandasi wamejitahidi kujenga Shule ya Sekondari ya Kata ya Milundikwa hadi kufikia

Kidato cha Sita lakini Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeamua Shule hiyo kuhamishwa mara moja kuanzia tarehe 1 Januari, 2017 ili kuliachia Jeshi:-

- (a) Je, Serikali inatoa mchango gani katika uhamishaji na ujenzi mpya wa Shule hiyo;
- (b) Je, Serikali iko tayari kufanya tathmini ya miundombinu yote ya Shule na majengo yaliyojengwa na Wananchi na thamani hiyo kuitoa katika fedha taslimu kwa ujenzi mpya wa Shule.

#### **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

#### **306. MHESHIMIWA MATTAR ALI SALUM (SHAURIMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:- Uvubi wa Bahari Kuu unaingiza kipato kikubwa sana na unaweza ukachagia katika bajeti ya nchi yetu:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kununua Meli za Uvubi;
- (b) Je, Serikali imefikia wapi katika ujenzi wa Bandari ya Uvubi nchini.

**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO  
WA AFRIKA MASHARIKI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**DODOMA**  
**23 MEI, 2018**

**S. KAGAIGAI**  
**KATIBU WA BUNGE**

